

Mkataba Wa Njia Bora

Kanuni 7 Za Njia Bora

1. **Tunafanya kazi kwa heshima bila nia ya kudhuru**

Tunajitahidi tunavyoweza kutii msimamo huu kama sheria, na kutunga kanuni katika huu mkataba zinazolingana nayo.

2. **Tunatambua ya kwamba sisi wanadamu ni viumbe huru na tunahiari pamoja na uwezo wa kujifanyia maamuzi**

Tunachukua jukumu la, na usukani wa, maisha, maamuzi na afya yetu kibinagsi.

3. **Sisi wanadamu ni viumbe vya kiasili**

Tunatambua ya kwamba ustawi wa watu na dunia unategemeana ndiposa tunakuza zote mbili kwa usawa.

4. **Binadamu anasehemu ya kiroho ambayo uzima wake ni muhimu kwa ustawi wetu**

Kwa kuwa watu ni wa kiroho, wanashamiri wakati wanafahamu maana na lengo kuu la maisha yao.

5. **Tunashamiri kwa kushirikiana pamoja**

Tunajumuisha watu wa nyanja tofauti na tunathamini jumuiya yetu inayounganisha na kushirikisha watu kutoka tabaka mbalimbali.

6. **Tunathamini mitazamo tofauti iliyopo**

Tunahimiza mijadala iliyopo na heshima kama njia mwafaka ya kuboresha maarifa, ubinadamu na hekima.

7. **Tunatumia teknolojia kwa busara tukitambua ya kwamba inafaida na hasara zake**

Tunatambua kuwa teknolojia inayotumiwa kwa heshima itaboresha elimu na hekima kwa manufaa ya wanadamu na dunia.

Kwa ujasiri tunapingga vikali:

- Ukiukaji wa haki za kibinadamu zisizoweza kutengwa pamoja na uhuru wa watu (uliofanuliwa humu*)
- Kuweka kipao mbele faida ya biashara, nguvu na ushawishi katika siasa ama ulimwengu kwa jumla, badala ya ustawi wa watu na dunia*

*Uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutembea sehemu mbalimbali, uhuru wa kukusanyika kwa kikundi; haki ya kujulishwa taarifa kamili, bila malipo, kuhusu dawa, utaratibu ama majoribio ya matibabu kabla ya anayehusishwa kupeana kibali iwapo atachagua kuidhinisha kushirikishwa; haki ya mwanadamu kudhibiti mwili wake kwa kujifanyia maamuzi kibinagsi; na kuwa, kila mtu anachukuliwa kama asie na hatia hadi kosa lake, iwapo analo, litakapothebitishwa.